

Mwongozo wa Gavana BRAD LITTLE kwa sisi wote kwa utaratibu wakubaki nyumbani

Updated March 25, 2020

Kujitenga

Wakaaji wote wa Idaho wanapashwa kujitenga wakibaki na kutumika kazi wakiwa nyumbani kwao Lakini kufwatana na utaratibu,wanao kubaliwa kutoka nje ni: Watoa huduma ya afia,ya usalama na wale wenyi shuruli muhimu.

Watu wakae nyumbani watapokea huduma muhimu unapo itajika

Hasara ni kubwa zaidi kwawenyi umri unaozidi miaka 65 na wanao matatizo ya afia.Wanaombwa wabaki nyumbani kwao.

Wafanya kazi wasiotoa huduma muhimu,wafanye kazi wakiwa nyumbani kwao

HUDUMA ZIFWATAZO ZITABAKI WAZI:

Soko,huduma ya afia,vituo vya mafuta (gas),benki ,duka za dawa,huduma za serkali,fasi ya kufuwa nguo, huduma ya matunzo za nyumbani ,huduma za mifugo,duga za vifaa vya kazi,utunzaji mdogo kwa wafanyakazi muhimu ,unjenzi Na huduma zingine muhimu inao ambatana na usalama na maisha bora wa wakaaji. Mikahawa(restaurants) zitaendelea na shuruli zao lakini wateja wasiingie ndani.Watapewa chakula wakiwa inje(drive thru)

HUDUMA ZISIZO ZAMUHIMU ZITAFUNGWA

Vyumba vya mazoezi,vifaa vya burudani,bar,vilabu vya usiku,kumbi za burudani,vituo vya mikusanyiko ,saluni za nyele na kucha,mikusanyiko za umma,kula kwenyi makahawa(restaurants) lakini wataendelea kupata chakula wakiwa inje na huduma zote ambazo azina umuhimu kulingana na utaratibu.

UPUNGUFU WA USAFIRI WA UMMA

Kwa wale tu wanaotoa ao kupata huduma muhimu

KUPUNGUZA USAFIRI

Acha usafiri usio walazima

MIKUSANYIKO

Punguza mikusanyiko ya watu nje ya nyumba yako Shuruli inje ya nyumba yako aikatazwi bali unapo karibia mtu asiekuwa wa nyumba yako simama naye ubali ya mita moja

MAZOEZI YA USAFI

Nawa mikono, Safisha mahali pote panapo guswa kila mara, Funika kinyua chako unapo kohowa ao kuchafia, Epuka jambo ya mikono.